*Kioo cha Lugha, Juz. 20(1), 36-49*
*Jarida la Taasisi ya Taaluma za Kiswahili*
*Chuo Kikuu cha Dar es Salaam* DOI: https://dx.doi.org/10.4314/kcl.v20i1.3

# Ubainikaji wa Aina za Ukatili wa Watoto katika Fasihi ya Kiswahili ya Watoto: Mifano kutoka Riwaya Teule

*Enock N. Nyariki*[1] *na Pamela Ngugi*[2]

**Ikisiri**

Makala hii imeangazia aina za ukatili wa watoto katika riwaya za Siku Njema (Walibora, 1996), Tumaini (Momanyi, 2006) na Lulu ya Maisha (Habwe, 2013) ambazo zinalenga hadhira ya watoto na vijana. Wachambuzi wengi wa fasihi ya Kiswahili ya watoto wamemwangazia mtoto kama mwathiriwa wa matendo ya ukatili. Kipengele cha mtoto kama mhusika katili ambaye matendo yake yanaweza kuwaathiri wanajamii wengine hakijahakikiwa kwa kina. Katika misingi hii makala iliangazia aina za matendo ya ukatili wa watoto katika vitabu teule vya fasihi ya watoto. Nadharia ya Uhalisia ambayo waasisi wake ni pamoja na Gustav Flaubert (1850), Rene Wellek (1963) na Lazaro Carreter (1970) ilitumika ili kuonesha jinsi ukatili wa watoto ulivyoakisiwa na waandishi. Data za msingi zilipatikana kwa kusoma vitabu teule. Aidha, makala ilinufaishwa kwa kuzisoma na kuzihakiki kazi zinazohusiana na mada hii kwenye majarida, magazeti, tasnifu, vitabu na machapisho mbalimbali. Maelezo ya kina yalitumiwa kuwasilisha matokeo ya utafiti. Aina tatu za ukatili zilijitokeza katika riwaya. Aina hizo ni ukatili wa kimatendo unaojibainisha katika matendo kama vile uvamizi, wizi na unyang'anyi; ukatili wa kimatamshi, ambao hubainika katika vitisho na matamshi ya kudhalilisha; na ukatili wa kifikra, ambao hujidhihirisha kwa ishara za maandishi, matamshi na kuwaandamaandama waathiriwa kwa nia ya kuwadhuru.

## 1.0 Utangulizi

Visa vya ukatili miongoni mwa watoto vimeongezeka katika siku za hivi karibuni na kulifanya suala hili kuwa mtambuka katika jamii (Connor, 2002; Khan, 2014; AACAP, 2015). Kulingana na Connor (2002), watoto wenye kasoro za kitabia mara nyingi husababisha migogoro katika familia zao na kuleta balaa shuleni ambapo walimu wao hujaribu kuzishughulikia kasoro hizo na kulinda usalama wa wanafunzi wenzao na wahusika wengine. Khan (2014) anaeleza kuwa ukatili ni

[1] Mwanafunzi wa Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Baruapepe: enocknyarikinyariki@yahoo.com
[2] Mhadhiri Mwandamizi, Idara ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika, Chuo Kikuu cha Kenyatta, Kenya. Baruapepe: NGUGI.PAMELA@ku.ac.ke

tatizo lililo dhahiri katika takribani asilimia 23-40 ya watoto ulimwenguni. Kwa mujibu wa AACAP (2015), watoto ambao hawajafikisha umri wa kwenda shuleni wanaweza kuonesha tabia za ukatili kwa sababu ya kuwa waathiriwa wa kuchapwa, kudhulumiwa kimapenzi, kushuhudia ukatili nyumbani na katika jamii, kutazama ukatili kwenye vyombo vya habari, na kuwa wahanga wa udhalilishaji, miongoni mwa sababu nyingine.

Ukatili wa watoto unadhihirika katika fasihi simulizi. Baadhi ya masimulizi, kwa mfano, hadithi, visasili, mighani, miongoni mwa mengine, yalijumuisha ukatili mwingi na dhuluma dhidi ya watoto (Morellato, 2017). Katika vitabu vya fasihi ya watoto, ukatili si suala geni, ila lina mizizi yake katika hadithi za kwanza walizoandikiwa watoto (Nimon, 1993; Todorova, 2020). Todorova (2020) anatumia mikusanyiko ya hadithi za kifantasia za Charles Perrault (1697) na Brothers Grimm (1812) kuonesha kuwa ukatili, jinsi unavyoeleweka sasa, ulikuwa jambo la kawaida katika maisha ya utoto na katika hadithi walizosimuliwa watoto tangu kale katika sehemu mbalimbali za dunia. Wataalamu hawa wanaeleza kuwa picha za matendo ya kikatili yanayosababisha uchungu kwa mwili zilitumika kama kielelezo cha nidhamu katika vitabu vya kufunzia watoto uadilifu. Nimon anahitimisha kwamba vitabu vya fasihi ya watoto vinaweza kushughulikia ukatili na migogoro ila vifanye hivyo kwa njia ambayo inaonesha majuto yanayotokana na adhabu inayopaswa kwa wahusika katili na suluhu ya ukatili wenyewe badala ya ulipizaji kisasi.

Koehnecke (2001) amechambua vitabu viwili vya picha vya watoto, *The House that Crack Built* (Taylor, 1992) na *Smoky Night* (Bunting, 1994). Vitabu hivi vinaangazia matendo ya ukatili ya watoto kama vile uporaji, uchomaji wa mali za watu na ulanguzi wa dawa za kulevya, jinsi yanavyojidhihirisha katika Jiji la Los Angeles. Koehnecke (2001) anaibua mitazamo mbalimbali ya wadau wa fasihi ya watoto kuhusu utumiaji wa vitabu hivi kuwafunzia wanafunzi wa gredi ya pili katika shule za Jimbo la Los Angeles. Wanaopinga matumizi ya vitabu hivyo kufunzia watoto wanalalamika kuwa vinayaangazia kwa uwazi mno masuala yanayozua hofu na yanayoweza kumwathiri mtoto kwa njia hasi (Alcorn, 1995; Krauthammer, 1995). Wanaounga mkono matumizi yake wanaviona vitabu hivyo kama nyenzo muhimu ya kupitishia maadili shuleni na kwenye jamii kwa misingi kwamba vinashughulikia masuala ambayo aghalabu wazazi hawayajadili na watoto wao (Diaz,1995).

Karanja (2008) ametafiti masuala ibuka katika hadithi za watoto na kuonesha jinsi waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya Kiswahili ya watoto walivyoangazia dhuluma dhidi ya watoto kama vile ubaguzi wa kijinsia, ukiukaji wa haki za watoto na unyanyapaa dhidi ya walemavu. Ingawa mtafiti ameangazia kwa namna fulani dhuluma zinazotekelezwa na watoto, kipengele hicho hakijaangaziwa kwa kina. Naye Kavuria (2008), ameangazia aina mbalimbali za dhuluma dhidi ya watoto kama vile kujeruhi kimwili na kihisia, unyanyasaji kimapenzi na kutowatunza watoto. Mwenda (2020) ametafiti kuhusu malezi katika

fasihi ya watoto ambapo amefafanua jinsi baadhi ya mbinu za malezi zinavyochangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto.

Watafiti wengi wamelishughulikia suala la ukatili katika fasihi ya watoto kwa mapana ingawa kipengele cha mtoto kama mhusika katili ambaye matendo yake yanaweza kuwaathiri wanajamii wengine hakijahakikiwa kwa kina. Katika misingi hii, utafiti huu ulikusudia kuangazia aina za ukatili wa watoto katika vitabu teule vya fasihi ya watoto ili kuliziba pengo lililopo na kutoa mchango muhimu kwa watafiti watakaoendeleza utafiti kuhusu mada hii.

## 2.0 Misingi ya Nadharia

Nadharia ya Uhalisia ilitumika ili kuelewa jinsi aina za ukatili unaotekelezwa na watoto zinavyoangaziwa kwa uyakinifu na waandishi wa fasihi ya watoto. Nadharia ya Uhalisia ilipata umaarufu mwanzoni mwa miaka ya 1850 ambapo dhana ya uhalisia na matumizi yake katika fasihi ilianza kujitokeza katika majarida ya Kiingereza kama vile *Fraser's Magazine* na *The Westminster Review* (Villanueva, 1997). Nadharia hii inahusishwa na wananadharia mbalimbali kama vile Rene Wellek (1961), Niebuhr Reinhold (1944) na Lazaro Carreter (1970). Villanueva (1997) anaelezea uhalisia kama dhana muhimu iliyoelekeza historia ya fasihi na ambayo hujitokeza katika fasihi zote. Anafafanua kwamba uhalisia ulijitokeza kwanza kama nadharia ya fasihi katika ushairi wa Aristotle uliojikita katika kanuni ya mwigo wa maisha.

Nadharia ya Uhalisia husisisitiza kwamba maisha ya jamii sharti yaangaziwe jinsi yalivyo (Wamitila, 2002). Wamitila (2002) anafafanua mhimili wa Nadharia ya Uhalisia unaoeleza kwamba mwandishi wa kazi ya fasihi husawiri picha ya wahusika, matukio na mandhari kwa njia inayoakisi jamii anamoishi. Mhimili huu ulisaidia katika kuelewa jinsi waandishi wa fasihi ya watoto walivyoakisi aina za ukatili wa watoto katika vitabu teule.

## 3.0 Mbinu za Utafiti

Makala ilitumia muundo wa kimaelezo katika kutoa ufafanuzi na ulinganishi wa aina za ukatili wa watoto zinavyoakisiwa katika riwaya teule za fasihi ya watoto. Utafiti wa kimaelezo hutoa ripoti ya jinsi mambo yalivyo katika mazingira fulani na hueleza tabia, mielekeo, itikadi na hali mbalimbali za watu (Mugenda na Mugenda, 1999). Utafiti ulijikita maktabani ambapo data za msingi zilipatikana kwa kusoma riwaya tatu teule ambazo ni *Siku Njema* (Walibora, 1996), *Tumaini* (Momanyi, 2006) na *Lulu ya Maisha* (Habwe, 2013). Data hizi ziligawanywa kwenye makundi na kuchambuliwa kwa kutumia mwongozo wa uchambuzi uliozingatia lengo la utafiti, nadharia husika na makala zingine. Maelezo ya kina yalitolewa kuhusu aina tatu za ukatili wa watoto unaojitokeza katika vitabu teule kwa kuelekezwa na nadharia husika.

## 4.0 Aina za Ukatili katika Riwaya Teule za Fasihi ya Watoto

Wataalamu mbalimbali wameeleza kuhusu yale yanayolifanya tendo kuitwa la kikatili (Stepanek, 2013; Leach, 2014; Chamandar na Jabbari, 2017). Kulingana na Stepanek (2013), kitendo kinaelezewa kuwa cha kikatili iwapo pana matumizi ya nguvu kwa nia ya kusababisha majeraha, maumivu ya kisaikolojia au kifo. Naye Leach (2014) anaeleza kuwa ili kitendo kiweze kufasiliwa kama cha kikatili ni sharti kiwe na nia ya kuumiza kimwili au kisaikolojia. Chamandar na Jabbari (2017) kwa upande wao wanafafanua kwamba kitendo cha kikatili hubainika kwa kuitazama dhamira ya mtendaji. Mtazamo wa wataalamu hawa ni kwamba kitendo kinakuwa cha kikatili iwapo dhamira ya mtendaji ni kujinufaisha mwenyewe kwa kupuuza haki za wengine. Kutokana na mitazamo hii, inabainika kwamba ukatili unaweza kujidhihirisha kwa matendo ya aina mbalimbali, baadhi yake yakiwa bayana kuliko mengine.

Kutokana na maelezo haya, ukatili umegawanywa katika makundi matatu ambayo ni ukatili wa kimatendo, kimatamshi na kifikra (Young, Boye na Nelson, 2006; Coyne, Archer na Eslea, 2006; Leach, 2014; Chamandar na Jabbari, 2017; Murray, Eisner na Ribeaud, 2018). Aina hizi za ukatili zilitambulika katika riwaya teule kupitia yale wanayoyafanya wahusika, kuyatamka au wasifu wa wahusika kuhusu wahusika wenza (Wamitila, 2002).

### 4.1 Ukatili wa Kimatendo

Kulingana na Young, Boye na Nelson (2006), ukatili wa kimatendo unahusu kusababisha majeraha au kutishia kusababisha majeraha. Sehemu hii iliangazia vipengele vinne vinavyohusu ukatili wa kimatendo ambavyo ni uvamizi kwa lengo la kulipiza kisasi au kutokana na hasira ya kudunishwa ama kutaka kujitetea; wizi na unyang'anyi; unyanyasaji wa kimapenzi na uharibifu wa mali.

Katika riwaya ya *Siku Njema*, Walibora (1996) anasimulia kuhusu Selemani, mwana wa Mapunda anayemvua nguo mkuu wa shule ya Tanga, kumpiga na kumjeruhi vibaya kwa kushirikiana na vijana wenzake. Mapunda anatekeleza kitendo hiki cha kikatili ili kulipiza kisasi dhidi ya mwalimu huyo ambaye awali alimwamrisha kuvua nguo na kuoga mbele ya wanafunzi na walimu waliokusanyika kwenye gwaride. Hivi ndivyo tukio la kupigwa kwa mwalimu linavyosimuliwa na Kongowea Mswahili:

> Yule mwanaume aliyepigwa na kugaragara chini uchi alikuwa mkuu wa shule wetu. Alikuwa kajeruhiwa vibaya kichwani. Damu ilimtoka kwa wingi. Kisha nikamuona Selemani. Macho alikuwa kayatoa pima na mkononi kashika kigongo huku majasho yanamtoka. Alihema kwa uchovu... (uk. 21).

Pokhrel na wenzake(2010) wanafafanua kuwa kumpiga mtu kwa kutumia silaha kama vile gongo, fimbo au kisu na kumsababishia majeraha ya kimwili ni ukatili. Mwandishi wa riwaya ya *Siku Njema* amekiakisi kitendo hiki kwa usahihi kwa

kuzingatia mhimili wa uhalisia unaoeleza kuwa waandishi wa fasihi ya watoto huyaakisi matendo kwa uyakinifu na uaminifu. Matendo haya hutokea mara kwa mara katika shule mbalimbali hasa nchini Kenya. Kwa mfano, katika gazeti la *The Standard*, Abuga (2021) anasimulia tukio ambapo mwanafunzi wa kidato cha tatu katika Shule ya Upili ya Kisii anasemekana kuwadunga walimu wawili kisu na kuwajeruhi vibaya. Mwanafunzi huyo alichukua uamuzi huo baada ya kuulizwa sababu iliyomfanya kuchelewa shuleni.

Katika riwaya ya *Tumaini* (2006) kinasimuliwa kisa cha Majuto, mwana wa Bwana Andrea, mwenye tabia inayotishia usalama wa wanafunzi na walimu katika Shule ya Kivulini. Wakati mmoja, Majuto anamvurumishia mwalimu mawe kupitia kwenye madirisha ya darasa lao. Mwalimu huyo anashurutika kujificha chini ya meza ili kuyakwepa mawe hayo yanayotupwa kwa kasi. Majuto anakitekeleza kitendo hiki ili kulipiza kisasi dhidi ya adhabu ya kuamrishwa na mwalimu huyo kupiga magoti mbele ya wanafunzi wenzake kisha kumfukuza nje ya darasa huku somo likiendelea. Ijapokuwa Majuto hakufanikiwa kumjeruhi mwalimu wake, kitendo hiki kinafasiliwa kuwa cha kikatili kwa sababu nia yake ilikuwa kujeruhi, kama anavyoeleza Onukwufor (2013:62):

> Mwuguzi ambaye anamdunga mgonjwa wake sindano chungu hawezi kusemekana kuwa mkatili kwa sababu hakuwa na nia ya kuumiza. Hata hivyo, mwanafunzi aliyemtupia mwenzake jiwe lakini likamkosa ni katili kwa sababu alikuwa na nia ya kujeruhi (Tafsiri ya watafiti).

Mwandishi wa riwaya ya *Tumaini* vilevile amekiakisi kitendo cha Majuto kwa uyakinifu na uaminifu ikizingatiwa kwamba matukio ya wanafunzi kuwatupia walimu wao mawe au kuwatishia kwa silaha hatari yamekuwa yakiangaziwa katika jamii na vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Katika gazeti la *The Daily Nation*, Ochunge (2021) anasimulia jinsi mwanafunzi wa darasa la sita katika Shule ya Msingi ya Shihumbi anavyosemekana kumuua mwalimu wake, Bw. Khataka, kwa kumpiga jiwe kwenye paji la uso kwa sababu marehemu alimzuia kuteka maji kwenye kisima chake.

Katika riwaya ya *Tumaini*, Tumaini anadhihirisha ukatili kwa kumrushia Kijungwe jiwe ambalo linaishia kumjeruhi mwalimu wao (uk. 73). Tumaini anatekeleza kitendo hiki kutokana na hasira ya kudhihakiwa na Kijungwe kwamba alitoroka tohara kwa sababu ya kuogopa kisu cha ngariba. Ijapokuwa kitendo cha Tumaini kilikuwa cha kujihami dhidi ya ushari wa Kijungwe, ni cha kikatili kwa kuwa ukatili si njia mujarabu ya kusuluhisha migogoro (Nimon, 1993). Nao Chamandar na Jabbari (2017) wanaeleza kuwa vitisho vya kujitetea dhidi ya ukatili unaoelekezwa kwako na mtu mwingine vinafasiliwa kuwa ukatili. Kitendo cha Tumaini kimeakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu kwa sababu picha ya wanafunzi kugeukia ukatili kama njia ya kujitetea dhidi ya ukatili wa wenzao au kusuluhisha migogoro baina yao hujitokeza aghalabu katika jamii. Ongwae (2021) anasimulia tukio ambapo mwanafunzi wa Shule ya Msingi Bogwendo katika

kaunti ya Nyamira anasemekana kumdunga mwenzake kisu na kumuua wakigombania kalamu ya wino.

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha* (2013), Fazul na Fatila, ambao waliingia katika ndoa wakiwa watoto wanapigana na kuumizana kwa sababu ya mambo madogomadogo (uk. 64). Kwa mfano, Fazul, aliyetarajiwa na Fatila kukidhi mahitaji ya chakula nyumbani, wakati mwingine alirudi mikono mitupu kwa sababu ya kukosa kibarua. Fatila, ambaye hakuelewa sababu ya mumewe kutonunua chakula, alimzomea; jambo hilo likaibua ugomvi. Kitendo hiki cha Fatila na Fazul kupigana ni cha kikatili kwa mujibu wa Onukwufor (2013).

Kwa ujumla, ukatili wa kimatendo unabainika kwa kiwango kikubwa katika riwaya teule. Aidha, ukatili huo unajitokeza kupitia matendo na masuala mbalimbali yanayojumuisha wizi na unyang'anyi, uharibifu wa mali na unyanyasaji wa kimapenzi. Masuala hayo na ukatili wa kimatendo yanabainishwa kama ifuatavyo:

### 4.1.1 Wizi na Unyang'anyi

Kwanza, ukatili wa kimatendo unajitokeza kupitia vitendo vya wizi na unyang'anyi. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Bakari, mwanawe Salim Makame, ananyakua kipochi cha mwanamke mmoja mtalii. Kitendo hicho kinaukasirisha umati wa watu ambao unampiga kitutu na kumuumiza. Maelezo mengine yanayotolewa na mhusika anayeitwa Rashid yanamsawiri Bakari kama mhusika sugu wa wizi ambaye anahatarisha maisha yake kutokana na tabia hiyo (uk. 64).

Katika riwaya hiyo ya *Siku Njema*, Selemani Mapunda na Bakari wanashirikiana katika kutekeleza vitendo vingi vya ungang'anyi na wizi wa kimabavu katika mji wa Mombasa na viunga vyake. Maelezo yanayotolewa kwenye gazeti la *Taifa Leo* punde tu polisi wanapowapiga risasi na kuwaua yanadhihirisha matendo hayo:

> Polisi waliwapiga risasi na kuwaua majambazi waliokuwa wakijaribu kuiba gari mjini Mombasa... Majina ya majambazi hao waliopigwa risasi mpaka kufa yalitolewa kama Bakari Salim na Selemani Mapunda. Selemani ni raia wa Tanzania. Wote wawili wanasemekana ni sugu wa jela ambao wamehusika katika visa vingi vya uhalifu (kur. 130-131).

Katika riwaya ya *Tumaini*, Majuto Kijungwe na kijana mwingine (hajatajwa jina) wanamwingilia mke wa mfanyabiashara anayeitwa Karim na kumkaba koo kisha wanamwibia kisanduku chenye vito.

Licha ya hayo, katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Omido, mwana wa Tiito, anawaibia watu mali zao. Majirani wa mtaa wa mabanda wa Kisera wanamwelekezea kidole cha lawama kwa kuleta magenge ya wezi yanayowaibia. Aidha, polisi wanaanzisha msako dhidi ya Omido na genge linalojiita RIZIKI kutokana na kisa cha wizi katika duka la Bwana Sultani.

Vitendo vya wizi na unyang'anyi vinavyodhihirika kupitia wahusika Mapunda, Bakari na Omido ambao wana umri wa takribani miaka kumi na minne katika riwaya teule za fasihi ya watoto ni ukatili. Hili linathibitishwa na Coyne, Archer na Eslea (2006) wanaoyafasili matendo kama vile kumnyang'anya au kumwibia mtu mali na kadhalika kuwa ukatili. Naye Felson (2009) anaeleza kuwa wizi na unyang'anyi ni ukatili kwa sababu wanyang'anyi na wezi huwatisha na wakati mwingine kuwajeruhi kimwili wahanga wao kama njia ya kupata wanachohitaji kwao. Jambo hili linabainika wakati Majuto, Kijungwe na wenzake wanapomkaba koo mke wa Karim ili kumwibia kisanduku chake chenye vito.

### 4.1.2 Uharibifu wa Mali

Kitendo kingine kinachodhihirisha ukatili wa kimatendo ni uharibifu wa mali ya mtu, kampuni, shirika, na kadhalika. Uharibifu wa mali ulioangaziwa na waandishi wa riwaya teule unatendeka pamoja na matendo ya wizi. Katika riwaya ya *Tumaini,* Majuto na Kijungwe wanavunja ofisi ya mwalimu mkuu, Bwana Mwadime, na kuiba madaftari wanayomuuzia Karim, mmiliki wa duka la jumla. Katika tukio jingine, Majuto na wenzake wanavunja ofisi ya D.O ili kuiba pesa. Wizi huu unatibuliwa na polisi ambao wanawafyatulia Majuto na Kijungwe risasi za miguuni na kuwatia mbaroni. Kwa mujibu wa Coyne, Archer na Eslea ( 2006), kumwibia mtu au kuharibu mali ni matendo ya ukatili. Naye Bourguignon (2000) anafafanua kuwa wizi, unyang'anyi na/au uharibifu wa mali hudidimiza uchumi, kusababisha umaskini na kutokuwapo kwa usawa, na hivyo basi, kutoa mwanya wa mzunguko wa visa vya ukatili miongoni mwa watoto.

### 4.1.3 Unyanyasaji wa Kimapenzi

Tukio lingine ambalo kwalo ukatili wa kimatendo hubainika ni unyanyasaji wa kimapenzi. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Selemani Mapunda anapotoroka shule anaelezewa kuwa alishiriki matendo mengi ya ukatili yakiwamo ubakaji wa mabinti wa watu. Maelezo sawa na hayo yanatolewa kumhusu mhusika Majuto wa riwaya ya *Tumaini*. Tukio moja ambalo linaonesha bayana kitendo cha ubakaji cha Majuto ni wakati anapojaribu kumbaka mhusika Tumaini. Kavuria (2008) anaeleza kwamba unyanyasaji wa kimapenzi hutokea mtu anapomshurutisha mwenzake kushiriki naye mapenzi au kumgusagusa kwa lengo hilo na kwamba hutokea na aina nyingine za ukatili. Naye Felson (2009) anaeleza kuwa wabakaji huwalazimisha wahanga wao kujisalimisha, ikiwa ndiyo njia ya pekee ya kupata wanachohitaji. Matendo ya wahusika hawa yameakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu na waandishi wa riwaya mbili teule.

Kwa ujumla, sehemu hii imeangazia ukatili wa kimatendo unaojidhihirisha kupitia uvamizi, wizi na unyang'anyi, uharibifu wa mali na unyanyasaji wa kimapenzi. Ukatili huu umeakisiwa kwa uyakinifu na uaminifu na waandishi wa vitabu teule vya fasihi ya watoto kwa sababu baadhi ya matukio ya watoto ambao

hutekeleza ukatili huu dhidi ya wahusika wengine huangaziwa katika vyombo mbalimbali vya habari nchini na kimataifa.

### 4.2 Ukatili wa Kimatamshi

Ukatili wa kimatamshi hujitokeza kwa njia ya matusi, kejeli, dhihaka na vitisho miongoni mwa mengine (Leach, 2014). Leach (2014) anafafanua kwamba wanaotekeleza ukatili huu hudhamiria kusababisha maumivu ya kisaikolojia kwa wenzao. Reyes (2007) anaeleza kwamba si rahisi kufasili dhana ya maumivu ya kisaikolojia kwa sababu matendo ambayo hukusudiwa kuumiza mwili pia yanaweza kuumiza hisia. Kulingana na mtaalamu huyu, maumivu ya kisaikolojia ni maumivu makali ya akili au mateso ambayo husababishwa na vitisho au matendo yanayodhamiriwa kuathiri utendakazi wa hisia au silika ya mtu. Reyes anaendelea kueleza kuwa maumivu ya kisaikolojia yanaweza pia kusababishwa kwa njia zisizosababisha majeraha ya kimwili au hata kugusa mwili lakini zinazogusa akili au hisia za mwathiriwa.

Ukatili wa kimatamshi katika riwaya teule za fasihi ya watoto unajidhihirisha kwa njia ya vitisho vya kutaka kulipiza kisasi na vya kujitetea dhidi ya ukatili unaoelekezwa kwa mwathiriwa. Pia, ukatili huu hujidhihirisha katika vitisho vya kutia woga kwa matakwa binafsi kama vile kutaka kufunika uovu fulani na matamshi ya kudhalilisha au ya hasira. Katika riwaya ya *Siku Njema,* Selemani Mapunda anaonesha ukatili kupitia maneno anayoyatumia kumrejelea hedimasta wao. Hivi ndivyo anavyosema: ‘‘Hili bwege leo litajua kilichomfanya sangara kuchomwa moto. Ati alitaka nioge mbele ya hadhara ile. Wallahi! Tutaliua hili. Na liwe liwalo” (uk. 21).

Maneno ya Selemani yanajumuisha vitisho na matusi yanayokusudiwa kulipiza kisasi kwa kumfanya mwalimu mkuu kukijutia kitendo chake cha awali cha kumwamrisha Selemani aoge mbele ya wanafunzi.

Katika riwaya ya *Tumaini,* Tumaini anamtishia Majuto kwa maneno yafuatayo: “Nikaribie uone ikiwa wewe kweli ni mwanamume. Unadhani kuwa mimi ni kama wale unaowavizia mitaroni!” (uk. 89).

Ingawa vitisho vya Tumaini vinakusudiwa kujitetea dhidi ya kitendo cha Majuto cha kutaka kumdhulumu kimapenzi, bado vinafasiliwa kuwa ukatili kwa mujibu wa Chamandar na Jabbari (2017). Wataalamu hawa wanaeleza kwamba vitisho anavyovitoa mwathiriwa ili kujitetea dhidi ya ukatili unaoelekezwa kwake pia huchukuliwa kuwa ukatili. Vitisho vingine vya kujitetea dhidi ya ukatili vinajitokeza katika riwaya ya *Lulu ya Maisha,* ambapo Sue anamtisha Maanzo kwa maneno, “Utaniona” (uk. 51). Sue anayatamka maneno haya kama njia moja ya kujitetea dhidi ya vitisho vya Maanzo ambaye anadhihirisha nia mbaya ya kumhujumu Sue kwa kukataa ombi lake la kutaka wawe wapenzi. Kwa kusema ‘utaniona,’ Sue alitaka kumthibitishia Maanzo kuwa hata yeye alikuwa na uwezo wa kumkabili na kujitetea dhidi ya vitisho vyake.

Katika riwaya ya *Siku Njema,* Selemani anamwambia Kongowea kwamba angemwua iwapo angeripoti kitendo cha kudhulumiwa kwa mwalimu mkuu kwa polisi (uk. 21). Vitisho hivi vinadhamiriwa kumtia Kongowea woga ili asiufichue uovu wa Selemani. Katika riwaya ya *Tumaini,* baada ya jaribio la Majuto la kumbaka Tumaini kutibuka, Majuto anamtishia kwa maneno yafuatayo: "Nitakuonyesha mimi ni nani siku moja" (uk. 89). Vitisho hivi vinadhihirisha kwamba Majuto alikuwa na nia ya kumvamia Tumaini katika siku za baadaye.

Licha ya hayo, katika riwaya ya *Tumaini*, Idi, mwana wa Mzee Masumbuko, anasawiriwa kama mtoto katili kutokana na matamshi yake ya kuwadunisha dada zake na jinsia ya kike kwa jumla. Idi anamwona Tumaini kama bidhaa ambayo punde si punde ingeuzwa ili baba yake apate pesa za matumizi. Anamwambia Tumaini waziwazi kwamba hata akikataa kufanyiwa tohara hatimaye angeolewa tu (uk. 29). Matamshi hayo yana dhamira ya kumdhalilisha Tumaini. Katika riwaya hiyo, Kijungwe anamuumbua Tumaini kwa kumwambia kuwa alikataa kutahiriwa kwa sababu ya kuogopa kisu cha ngariba au kwa sababu ya kutompenda mchumba ambaye tayari alikuwa amechaguliwa (uk. 72).

Matamshi mengine ya ukatili yanajitokeza katika mazingira ya shuleni. Katika riwaya ya *Siku Njema*, baadhi ya wanafunzi wa darasa la Kongowea wanamdhalilisha anapowashinda katika mtihani kwa kumwita majina kama kitoto kichekechea, kikojozi na mwanaharamu. Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Sue anakuwa mwathiriwa wa vitendo vya ukatili vya wanafunzi wa shule ya St. Mary's Girls Primary Boarding wanaomwamrisha kuimba kidogo, kulia na kuwasifu wale ambao walikuwa viranja wao. Udhalilishaji wa wanafunzi dhidi ya wenzao umetafitiwa na Itegi (2017). Mtafiti anaeleza kuwa wanafunzi huwadhalilisha wenzao kwa kuwatusi na kutishia kusababisha majeraha miongoni mwa njia nyingine.

Katika riwaya ya *Tumaini*, baadhi ya wanafunzi wa kike wa shule ya Kivulini ambao hawafaulu katika masomo ya sayansi wanaonesha ukatili kwa walimu wa masomo hayo kupitia matamshi ya hasira na chuki. Almasi ni mmoja wa wanafunzi hao ambao wanamchukia mwalimu wa somo la Hisabati bila sababu (uk. 73). Kulingana na Chamandar na Jabbari (2017) kutamka maneno ya hasira kuhusu mtu mwingine au kwa mtu mwingine ni ukatili.

Kwa jumla, sehemu hii imeangazia ukatili wa kimatamshi wa watoto unaojitokeza kupitia vitisho vya kulipiza kisasi, vya kujitetea dhidi ya ukatili unaoelekezwa kwa mtu mwingine, vya kutia woga kwa matakwa fulani, matamshi ya kudhalilisha na ya hasira. Ukatili huu ambao hudhamiriwa kuathiri kisaikolojia umeakisiwa na waandishi wa vitabu vitatu teule kwa uyakinifu na uaminifu.

### 4.3 Ukatili wa Kifikra

Aina nyingine ya ukatili inayojibainisha katika riwaya teule ni ukatili wa kifikra. Leach (2014) anafafanua kuwa ukatili wa kifikra ni hali ya kufikiria, kupanga

njama au kitendo cha ukatili bila kukitekeleza kitendo chenyewe. Ukatili huo pia unaelezewa kuwa ni mawazo au fikra za kifantasia za kumjeruhi mtu mwingine (Murray, Eisner na Ribeaud, 2018). Hata hivyo, si rahisi kuyatenganisha matendo ya ukatili wa kifikra kwa kuwa baadhi yake hutokea kwa pamoja.

Katika riwaya teule, ishara mbalimbali zinaonesha kuwa wahusika fulani wanafikiria kutekeleza ukatili dhidi ya wenzao. Ishara hizi zinajidhihirisha kwa njia ya matamshi, maandishi, kumiliki silaha hatari na kuwaandamaandama wahanga kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa nia ya kuwadhuru miongoni mwa nyingine. Katika riwaya ya *Siku Njema*, Selemani anatishia maisha ya Kongowea kupitia barua anayomwandikia katika mji wa Tanga mara tu anapotoka jela:

> *Kwa kongoweya Muswahili,*
> *Uliniponza nikafungwa jera. Sasa nimetoka jera.*
> *Utakiona cha mutema kuni. Taree 31 julai 1971*
> *muaka uu nitakuua.Selemani* (uk. 33).

Baadaye, Selemani anatiwa mbaroni na polisi akiwa na bastola aliyopanga kuitumia kutekeleza vitisho alivyowasilisha kwenye barua. Fauka ya hayo, Selemani anapotoroka jela anakimbilia Mombasa kwa nia ya kumsaka na kumwangamiza Kongowea kama inavyodhihirika kupitia ujumbe anaoandika kwenye choo cha wapangaji katika mji huo unaosomeka:

> *Kongoweya wewe ndiye ulini haripiya bahati yangu,*
> *ulipokimbilia Mwambasa ulifikili sitokupata. Nitakuua.*
> *Niko apa mjini. S.M.* (uk. 100).

Matendo ya Selemani yameangaziwa kihalisia na mwandishi kwa sababu visa vya wanafunzi waliopatikana na silaha hatari ambazo hudhamiria kuzitumia kutekeleza uhalifu shuleni yamewahi kuangaziwa na vyombo vya habari nchini Kenya. Kwa mfano, Mugo (2021) anasimulia tukio ambapo mwanafunzi wa shule ya upili ya David Kamana katika kaunti ya Embu anatiwa mbaroni kwa kupatikana na risasi shuleni. Katika tukio hilo, mlinzi wa shule alipoingia kwenye bweni alipolala mwanafunzi huyo, alikumbana na moto uliowashwa kwa kutumia karatasi, jambo linaloashiria kuwa alikuwa amefikiria kuchoma bweni.

Katika riwaya ya *Lulu ya Maisha*, Sue anadhihirisha ukatili anapotishia kuchukua shoka ili akawakabili ami zake wanaowanyang’anya urithi walioachiwa na marehemu baba yao. Hata hivyo, hakitekelezi kitendo chenyewe kutokana na maonyo ya mama yake ambaye anamshauri kwamba ilikuwa vibaya kuwaza mabaya dhidi ya ami zake.

Kwa ujumla, sehemu hii imeangazia ukatili wa kifikra ambao unaweza kujidhihirisha kupitia ishara ya matamshi, maandishi, kumiliki silaha hatari na kuwaandamaandama wahanga kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa nia ya kuwadhuru miongoni mwa nyingine. Visa hivi vimeakisiwa kihalisia na waandishi wa riwaya teule za fasihi ya watoto kwa uhalisia kwa sababu yapo baadhi ya

matukio yaliyowahi kuangaziwa na vyombo vya habari. Mathalani, katika gazeti la *Daily Nation*, Oduor (2017) anaripoti tukio ambapo mwanafunzi wa shule ya upili ya Orero, kaunti ya Homa Bay alitiwa mbaroni aliposemekana kupatikana na bastola shuleni aliyoitumia alipotaka kuwalazimisha wanafunzi wenza kutimiza matakwa yake.

## 5.0 Hitimisho

Waandishi wa riwaya teule za fasihi ya watoto wameangazia aina mbalimbali za ukatili unaotekelezwa na watoto dhidi ya wahusika wengine kwa njia ya uhalisia. Aina hizi za ukatili hudhihirika mara kwa mara katika jamii ambapo huangaziwa na vyombo mbalimbali vya mawasiliano. Lengo la utafiti lilikuwa kusahihisha dhana ambapo jamii humchukulia mtoto kama mhanga tu wa matukio ya ukatili. Mtoto pia ni mhusika katili ambaye matendo yake yanaiathiri jamii kwa njia mbalimbali. Katika misingi hii, utafiti umetoa mchango kwa watafiti wengine watakaoendeleza utafiti kuhusu mada hii kuchunguza sababu zinazochangia tabia ya ukatili miongoni mwa watoto, athari ya matendo ya watoto hao kwa wanajamii wengine na kupendekeza mikakati mbalimbali ya kuikabili tabia hiyo ya ukatili.

## Marejeleo

AACAP. (2015). Violent Behaviour in children and Adolescents. American Academy of child and Adolescent Psychiatry Juzuu. 55. Inapatikana katika https://www.aacap.org. Imesomwa tarehe 16 Machi 2022.

Abuga, E. (2021). Student Stabs Two Teachers at Kisii School. *The Standard*. Inapatikana katika https://www.standardmedia.co.ke. Imesomwa tarehe 28, Februari, 2022

Bourguignon, F. (2000). "Annual World Bank Conference on Development Economics 1999." Katika, B. Pleskovic na J. Stiglitz (Wah.), *Crime, Violence and Inequitable Development.* Washington DC The: World Bank. Kur.199-220.

Chamander, F. na Jabbari, S. (2017). Analysis of Component of Aggression in the Stories of Elementary School Children. *Journal of Education and Learning.* 6(2):187-195. Doi:10.5539/jel.v6n2p187. Imesomwa tarehe 27 Februari 2022.

Connor, D. F. (2002). "Prevalence of Aggression, Antisocial Behaviors, and Suicide in in Children and Adolescents." Katika, D.F. Connor (Mh.), *Aggresion and Antsocial Behaviuor in Children and Adolescents: Research and Treatment*. New York: Guilford. Kur. 28-45.

Coyne, S., Archer, J. na Eslea, M. (2006). "We're Not Friends Anymore! Unless… The Frequency and Harmfulness of Indirect, Relational, and Social Aggression." *Official Journal of International Society for Research on Aggression.* 32:294-307. Inapatikana katika https://onlinelibrary.wiley.com/doi/epdf/10.1002/ab.20126. Imesomwa tarehe 10 Februari, 2022.

Donnelly, J. (2000). *Realism and International Relations*. New York. Cambridge University Press.

Felson, R. (2009). "Violence, Crime, and Violent Crime." *International Journal of Conflict and Violence.* 3(1): 23-39. Inapatikana katika https://doi.org/10.4119/ijcv-2791. Imesomwa tarehe 16 Februari, 2022.

Gachuhi, K. (2019). "Shock, Tears as Two Students Held Over Killing." *The Standard.* Inapatikana katika https://www.standardmedia.co.ke/. Imesomwa tarehe 17 Oktoba, 2022.

Habwe, J. (2013). *Lulu ya Maisha*. Nairobi. The Jomo Kenyatta Foundation Publishers.

Itegi, F. (2017). Bullying and its Effects: Experience in Kenyan Public Secondary Schools. *International Journal of Education and Research*. 5(3). Inapatikana katika https://ir-library.ku.ac.ke/bitstream/handle/123456789/18209. Imesomwa tarehe 4 Machi, 2022.

Karanja, D. (2008). Usawiri wa Masuala-ibuka katika Hadithi za Watoto. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Kavuria, P. (2008). Dhuluma Dhidi ya Watoto katika Riwaya za Kiswahili. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Khan, M. (2014). "Association of Family Structure and its Environment with Aggressive Behaviour of Children (6-8years) in a Rural Community." *Journal of Child and Adolescent Behaviour*. 2(01):8-11. Inapatikana katika https://doi.org/10.4172/jcalb.1000125. Imesomwa tarehe 11 Januari, 2022.

Koehnecke, D. (2001). "Smoky night and crack: Controversial Subjects in Current Children's Stories." *Children's Literature in Education.* 32(1):17–30. Inapatikana katika https://doi.org/10.1023/A:1005261920692. Imesomwa tarehe 12 Machi 2022.

Leach, K.D. (2014). Aggression in Popular Children's Picture Books: Content Analysis. Brigham Young University. Tasnifu ya Umahiri (Haijachapishwa). Inapatikana katika https://scholarsarchive.byu.edu/etd/4102. Imesomwa tarehe 28 Februari, 2022.

Momanyi, C. (2006). *Tumaini.* Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Morellato, L. (2017). Symbolic Violence in Contemporary Japanese Children's Literature: Case study of a Japanese Folktale in its 21 Century Picture Book Renditions. (Working papers in contemporary Asian studies; No. 58). Centre for East and South-East Asian Studies, Lund University.

Mugenda, O. na Mugenda, E. (1999). *Research Methods*: *Quantitative and Qualitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mugo, M. (2021). Boy Caught with Ammunition in School. *The Standard*. Inapatikana katika

https://www.standardmedia.co.ke. Imesomwa tarehe 17 Oktoba, 2022.

Murray, A.; Eisner, M.; Ribeaud, D. (2018). "Development and Validation of a Brief Measure of Violent Thoughts: The Violent Ideations Scale (VIS)." *Assessment*. 25(7): 942-955. DOI: Inapatikana katika https://doi.org/10.1177/1073191116667213. Imesomwa tarehe 22 Januari, 2022.

Mwenda, A. (2020). Taswira ya Malezi ya Watoto katika Riwaya za *Tumaini* (2006) na *Dunia Mashaka Makuu* (2004). Tasnifu ya Uzamili (Haijachapishwa). Chuo Kikuu cha Kenyatta.

Nimon, M. (1993). Violence in Children's Literature Today. Katika, M. Nimon (Mh.), Annual Conference of International Association of School Librarianship. Adelaide, South Australia: US Derpatment of Education. Kur. 27-30.

Ochunge, N. (2021). Class Six Pupil Kills Teacher After a Fight Over Water. *The Standard*. https://www.standardmedia.co.ke/. Imesomwa tarehe 28 Machi, 2022.

Oduor, B. (2017). Shock as Student Arrested for Keeping Gun in School. *The Daily Nation*. Inapatikana katika https://nation.africa/kenya/news/. Imesomwa tarehe 30 Februari, 2022.

Omoteso, B.A. (2010). "Bullying Behaviour, its Associated Factors and Psychological Effects among Secondary School Students in Nigeria." *Journal of International Social Research.* 3(10) 498-508.

Ongwae, S. (2021). Class Seven Pupil in Nyamira Stabs Classmate to Death Over a Pen. *The Standard*. Inapatikana katika https://www.standardmedia.co.ke/western/article/2001413826. Imesomwa tarehe 28, Machi 2022.

Onukwufor, J. (2013). "Physical and Verbal Aggression among Adolescent Secondary School Students in Rivers State of Nigeria." *British Journal of Education.* 1(2) 62-73.

Inapatikana katika https://d1wqtxts1xzle7.cloudfront.net. Imesomwa tarehe 4 Februari, 2022.

Pokhrel, P., Sussman, S., Black, D. na Sun, P. (2010). "Peer Group Self-identification as a Predictor of Relational and Physical Aggression among High School Students." *Journal of School Health.* 80(5):249-258. Inapatikana katika https://onlinelibrary.wiley.com/doi/10.1111/j.1746-1561.2010.00498.x. Imesomwa tarehe 2 Februari, 2022.

Reyes, H. (2007). "The Worst Scars are in the Mind: Psychological Torture." *International Review of the Red Cross*. 89 (867): 591-617. Inapatikana katika https://www.icrc.org/en/doc/assets/files/other/irrc-867-reyes.pdf. Imesomwa tarehe 18 Februari, 2022.

Stepanek, P. (2013). Acts of Violence in English Fairy Tales Collected by Joseph Jacobs. Brno. Masaryk University. Bachelor's Diploma Thesis (Haijachapishwa). Inapatikana katika https://is.muni.cz/th/nnonh/?kod=e008. Imesomwa tarehe 28 Septemba, 2021.

Todorova, M. (2020). Translating Violence in Children's Picture Books: A View from the Former Yugoslavia. Katika C. Jan na M.M. Jack (Wah.), *Children's Literature in Translation: Texts and Contexts.* Leuven: Leuven University Press. Kur. 249-262.

Villanueva, D. (1997). *Theories of Literary Realism.* New York: State of New York Press, Albany.

Walibora, K. (1996). *Siku Njema*. Nairobi: Longhorn Publishers (k) Ltd.

Wamitila, K. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Young, E., Boye, A. na Nelson, D. (2006). Relational Aggression: Understanding, Identifying and Responding in Schools. *Wiley Periodicals*. 43(3). DOI: 10.1002/pits.2014. Imesomwa tarehe 13 Februari, 2022.